**Ndege Hawakutokana na Wanyama Wakubwa;**

Hebu nikwambie kuhusu kitabu nikipendacho. Kitabu chenyewe kinaitwa Biblia! Kitabu cha ajabu, kilichoandikwa ili tumjue Muumba, 1 Yohana 5:11-13. Kilichoandikwa ili tujue tunachopaswa kufanya ili “tuwe na uzima wa milele,” 1 Yohana 5:11.

Ukifungua Biblia katika Mwanzo 1:1, twasoma kwamba “Hapo mwanzo Mungu aliumba mbingu na nchi.” Naona ajabu kuona kuwa Mungu hakutunga hadithi hii ili kuthibitisha uwepo wake. Alieleza tu, “Niko.” Kama alivyomwambia Musa katika Kutoka 3:14, “Mimi NIKO ambaye NIKO.” Na kila mtu ana utashi, Yoshua 24:15; Kumbukumbu 30:19. Kwa hiari mtu anaweza kuchagua kumkubali Mungu au kukataa kabisa wazo la uwepo wa Mungu. Kwa sasa, Warumi 14:11.

Kwa sasa kukataa uwepo wa Mungu, Muumba wetu, ni ujinga. Unaona? Ujinga unamaanisha tu “ukosefu wa maarifa, elimu, au uelewa.” Hivyo, wengine ni wajinga. Nimefikia hatima hiyo kwa sababu ushahidi unatupeleka huko! Kama vile Warumi 1:20 na Matendo ya Mitume 14:16-17 inavyofundisha kuwa Mungu hakujiacha pasipo ushuhuda! Unataka ushahidi kwamba ulimwengu uliumbwa? Mungu anatupa ushahidi: mvua, majira ya mazao na vitu vionekanavyo dhahiri. Vionekanavyo dhahiri! Swali ni: uko tayari kuona? Au kiburi na noti vinakupofusha macho yako?

Ngoja nikwambie kuhusu ya timu yangu niipendayo ya chuo. OSU! Buckeyes ya Ohio! Napenda kusikia, kuona na kusoma kuhusu OSU. Lakini unajua nini? Mwaka jana ushahidi ulipothibitisha kwamba buckeyes haikuwa timu bora nchini, niliupokea ushahidi huo. Ilikuwa vigumu kuukubali, lakini ndugu zangu kadhaa walinisaidia na wengine walinicheka. USC iliifunga OSU. Kwa hiyo, nilikuwa na uamuzi. Ningeweza kuukubali ushahidi uniongoze ama ningeukana ili nionekane mjinga. Hata katika sayansi wangeweza kufanya hivi hivi. Wangeweza kusema “OSU ndiyo timu bora ya chuo kwa muda wote kwa mwaka 2008/2009.” Kisha baada ya maelezo hayo wangeweka alama hii “*” ikifuatiwa na maandishi madogo, “Lakini USC imewatungua vibaya.” Jambo la msingi hapa ni kwamba wanasayansi na makumbusho wanapenda alama “*” kuliko kueleza ukweli tu.

Sasa, ngoja nikwambie kuhusu OSU nyingine, Chuo kikuu cha Jimbo la Oregon ( najua wengine niliwakwaza, lakini nyinyi sio Buckeyes). Nakwambia haya kwa sababu katika gazeti la ScienceDaily (juni 9, 2009) unaweza kuisoma taarifa iliyotolewa hivi karibuni, ikizungumzia ushahidi uliotolewa na Chuo Kikuu cha Oregon kwamba ndege walitokana na Wanyama wakubwa. Je, ndiyo kusema kuwa naamini kuwa msimamo wa wana mageuzi na mageuzi hapa Marekani utabadilika ili wakubali ushahidi huu? Hasha! Na sababu ni kwamba kuna fedha nyingi na ajira nyingi zilizoko katika mfumo wa mageuzi kuliko wao kukubali ukweli na kuipokea hali halisi. Wataweka tu alama nyingine ya “*” nyuma ya uongo wao.

Ruben alisema, “lakini nadharia za kale huchukua muda kufa, hasa hasa linapokuja suala la viumbe wa aina tofauti katika historia ya ulimwengu. ‘Kiukweli, kuna siasa za makumbusho zilizohusishwa katika hili, wana taaluma wengi wamejitolea kushughulikia

mtazamo huu huu hata kama ushahidi mpya wa kisayansi unaibua swali “ mh! Hivi si nimesema tu?”

Kwa mujibu wa watafiti kutoka katika OSU ndogo, wamegundua na kuja na jawabu ambalo litawafanya wataalamu wa elimu mambo kale wajutie kusikia. Jawabu ni: (Sasa hili hutalisikia katika PBS, au katika minadi mingine ya kiliberali kwa sababu wanatakiwa kulinda kitu chao.) Ndege <u>hawakuzaliwa</u> kutokana na ukoo wa wanyama wakubwa. Wanamageuzi wamekuwa wakiudanganya umma wa Wamarekani kwa miaka mingi kwamba kwamba ndege wametokana na Wanyama wakubwa. Nenda kaangalie vitabu wanavyosomea watoto wenu shuleni. Lakini kwa sasa Sayansi imethibitisha kuwa ndege <u>hawakutokana</u> na wanyama wakubwa

Jawabu jipya linajikita katika namna “wanavyopumua na walivyo na uwezo kwenye mapafu unaowawezesha kupaa.” “ Labda ugunduzi huu unamaanisha kuwa ndege walifuka katika njia sambamba pembeni mwa wanyama wakubwa, huku ndege wakiwa wameanza hatua hiyo kabla ya wanyama wakubwa walio wengi kuwako duniani,” Alisema John Ruben wa OSU, Ili kusoma zaidi kuhusiana na taarifa hii, tafadhali tazama jarida la “The Journal Publication.”

Jawabu hili jipya linatokana na ukweli kwamba mfupa wa paja la ndege umerekebika, na sasa wanakimbia kutokea katika magoti na chini sawa sawa na wanyama wa nchi kavu. Mfupa wetu wa paja hutuwezesha kutembea, kukimbia na katika mfumo wa kujongea. Kwa hiyo, kwa kule kuwa ndege wana mfupa uliorekebika, ndege wanaweza kuuongezea nguvu muundo pekee wa mapafu unaosaidia mapafu yasichoke wakati wa kupumua. “Watafiti walisema, jambo hili ni ushahidi kuwa ndege hawakutokana na wanyama wakubwa. Matokeo yanaongezea ushahidi kwa takribani miongo miwili, ushahidi ambao unakosoa itikadi iliyosadikiwa na watu wengi kuhusiana na mageuzi ya wanyama.

Je ndiyo kusema naamini kwamba chombo chetu kikubwa huru cha habari hapa Marekani, majuma machache yajayo kitaanza kutangaza kuhusu huu ugunduzi mpya? Hasha! Hii ni kwa sababu tayari sayansi imeshatangaza kuwa ndege walitokana na wanyama wakubwa. Lakini bado ushahidi unaonyesha nini?. Ushahidi unaonyesha kuwa OSU ilishinda katika mchezo wa kuwania ubingwa wa Taifa mnamo 2009! Si ndiyo? Nenda wewe Buckeyes! Hapana! Basi kubali kwamba OSU walifungwa. Nilikubali, ingawaje inauma. Bado, wana mageuzi hawawezi kukubali kosa katika jambo hili kwa sababu kufanya hivyo kutawafanya wapoteze uso wao na pesa!

Hivyo, kama unamkabili mwana mageuzi kuhusu hili, mwingine atasema, sawa, lakini hili ni la ghafla.. Kweli eti! Lakini ni moja ya idadi inayoongezeka ya mambo ya ghafla yanayoibuliwa kila uchao ambayo yanaipinga imani ya ki-Darwin. Tatizo ni kiburi, pesa, na yote kwa pamoja yamefungamanishwa katika U-darwin kwa wana mageuzi kukubali makosa.

Sasa Biblia inasemaje kuhusiana na haya yote? Biblia inasema katika siku ya tano ya uumbaji, Mungu aliumba ndege na samaki na kuwaamuru wakazaliane, Mwanzo 1:20-23. Biblia inasema katika siku ya sita, Mungu aliwaumba wanyama waendao juu nchi na

akaona ni vyema, Mwanzo 1:24-25. Pia, siyo kweli kwamba sisi (wakristo) tulihitaji mtu aje kututhibitishia haya, kwa sababu tunaenenda kwa imani, 2 Wakorintho 5:7. Lakini watu wengine wanatakiwa waone ushahidi ndipo waamini, na kwa bahati yao, Mungu amewapa ushahidi. Lakini wataamini Ubingwa wa OSU mwaka 2009!

"Sasa inaonekana waziwazi kuwa ndege walikuwa wakizaliana kwa jinsia yao na hawakutokana moja kwa moja na wanyama wakubwa" Asante sana OSU mdogo, endelea kuchimbua!